

*Shairi hili lifuatalo ni la Ustadh Amiri A.S. Andanenga (Sauti ya Kiza) alilolitunga na kulisoma hadharani wakati wa uzinduzi wa kongomano la sera ya utamaduni, jijini Dar.*

### **SERA YA UTAMADUNI (UZINDUZI)**

1. Kwa hadhi na taadhima, nasimama hadharani.  
Akina baba na mama, naomba nisikizeni.  
Kwenu nitakayosema, kwa kina zingatieni.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
2. Iwapo halitakufa, huwa halina thamani.  
Litaisha kwa kashifa, kwa kuiga ya kigeni.  
Na hiyo ndiyo maafa, tuyaepuke jamani.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
3. Baada ya kujadili, kwa ndani utafitini.  
Tukagundua ukweli, ambao ni wa yakini.  
Ndipo kongomano hili, hapa likawaiteni.  
Huwa Taifa duni, liso na Utamaduni.
4. Leo ndio uzinduzi, "Sera ya Utamaduni".  
Ili kuiweka wazi, ieleweke Nchini.  
Pia ifanyiwe kazi, isibaki vitabuni.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
5. Kama tukiulizana, "Utamaduni ni nini?".  
Majibu yatagongana, kutoka mwetu vichwani.  
Mbali hayataachana, kwenye yake tathmini.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
6. Utamaduni matendo, hupokewa Taifani.  
Na kisha yake mitindo, huenea majimboni.  
Yalo na mwema mwenendo, hupokewa Taifani.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
7. Upo ule wa maisha, wa viumbe duniani.  
Mfano wa kunyonyesha, kwa wote hatuachani.  
Ujumbe kuufikisha, kwa lugha hatulingani.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
8. Tatizo huanza hapa, shina kwenda kileleni.  
Ikiwa mtaitupa, lugha yetu jalalani.  
Wote mtatapatapa, sawa wafao majini.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
9. Sisi kwa hali na mali, vibwebwe tujifungeni.  
Hata iwe bei ghali, tuikabili medani.  
Tutetee Kiswahili, kiwe mbele maishani.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
10. Rangi mtu hujulisha, atokako kwa kudhani.  
Pengine hukupotosha, sivyo ulivyobaini.  
Lugha inathibitisha, utaiifa kwa bayani.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
11. Lugha sitetei tuu, sababuye ishikeni.  
Lugha ndiyo zana kuu, kwa yote ulimwenguni.  
Lugha ipandishwe juu, ufuzu Utamaduni.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
12. Kiswahili himahima, kifundishie shuleni.  
Kipate yake heshima, kifundishie vyuoni.  
Nguo tunazoazima, hazihifadhi mwilini.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
13. Lugha nyingine masomo, zitieni vipindini.  
Na Kiswahili kiwemo, mbinu zake kazieni.  
huo ndiwo msimamo, wa kututia "utuni".  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
14. Kwamba hakitoshelezi, kamwe sikubaliani.  
Lugha gani zako njozi, waota usingizini?  
Maneno ya uchafuzi, tuyatupie mbalini.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
15. Yamepitwa na wakati, "eti" yote ya zamani.  
Ya sasa ni madhubuti, yote tusiyaamini.  
Kubwia mihadharati, "usasa" mwaunenani?  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
16. Kamwe si vyote dhahabu, ving'aravyo minadani.  
Nazo shaba zaghibu, zinazwa madukani.  
Zishawatia aibu, walovaa harusini.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
17. Mpingo mti mweusi, waota Afrikani.  
Unauzwa kwa fulusi, ghali sana duniani.  
Kudharau yetu sisi, tunatiwa ujingani.  
Huwa ni Taifa duni, liso na Utamaduni.
18. Usemi wangu nifunge, wajumbe wetu Bungeni.  
Sera hii muiunge, ili ipate mizani.  
Nasi raia tuchange, mazuri yatuauni.  
Lisiwe Taifa duni, liwe na Utamaduni.

*Amiri A.S. Andanenga (Sauti ya Kiza)  
Kinondoni - Shamba  
Dar es Salaam  
Tanzania.*